

**HOTUBA YA KATIBU TAWALA MKOA WA MARA
KATIKA UFUNGUZI WA KIKAO CHA KUJADILI
UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA AFYA YA UZAZI
NA MTOTO MKOA WA MARA UKUMBI WA MCN-
TARIME MJINI TAREHE 28-29/05/2018**

Mwakilishi wa OR- TAMISEMI

Mganga Mkuu Mkoa wa Mara

Timu ya Usimamizi wa Huduma za Afya Mkoa

Waganga Wakuu wa Halmashauri

Wadau wetu Jhpiego na washirika wake wote mliko hapa

Mganga Mkuu Hospitali ya Rufaa ya Mkoa - Musoma

Timu ya Usimamizi wa Huduma za Afya za Halmashauri

Watumishi wote kutoka vituo vya kutolea huduma za Afya

Mabibi na mabwana,

Asalaam aleikum.

Ndugu washiriki

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutupatia uhai na afya njema kufikia siku na kuweza kujumuika pamoja katika kikao hiki muhimu cha kujadili utekelezaji wa shughuli za afya ya uzazi na mtoto mkoa wa Mara. Pili ninawashukuru kwa kunialika ili nifungue kikao hiki, hii ni nafasi nzuri kwangu kwani napata nafasi ya kuongea na ninyi tena.

Ninaipongeza timu ya usimamizi wa huduma za Afya ya Mkoa na Halamashauri zote kwa kuendelea kuratibu shughuli zote za Afya katika Hal mashauri na Mkoa kwa ujumla. Niwashukuru pia kwa maandalizi ya kikao hiki muhimu; kipekee niwashukuru Wadau wetu wetu USAID Boresha Afya.

Ninyi mnafanya kazi kubwa katika Mkoa wetu hasa kwa upande wa afya ya uzazi na mtoto lakini pia

nimeambiwa kikao hiki gharama zote mnazitoa ninyi.
Ahsanteni sana.

Ndugu washiriki

Kikao hiki ni cha siku mbili, leo na kesho, naomba tutambue vikao kama hivi ni muhimu sana kwa kuwa vinatumika kuwapima kwa kazi mnazozifanya katika Halmashauri na vituo vyenu. Nimeelezwa kwamba kila Halmashauri itawasilisha utekelezaji wa viashiria mbali mbali vya afya ya uzazi na mtoto kwa vipindi viwili vya Oktoba – Desemba 2017 na Januari- Machi 2018.

Naomba nitumie nafasi hii kuwakumbusha, viashiria hivi mtakavyowasilisha na kujadili ndivyo vile vinavyotumika kuwapatia fedha za mfuko wa pamoja (Busket fund) ambazo sasa zinaletwa moja kwa moja kwenye vituo vyenu.

Baadhi ya viashiria hivyo ni:

- Idadi akina mama wajawazito chini ya wiki 12 walio hudhuria kliniki

- Idadi ya waliopimwa ugonjwa wa kaswende na kupata matibabu
- Waliopimwa ugonjwa Malaria kwa hudhurio la kwanza
- Idadi ya akina mama waliojifungulia katika vituo vya kutolea huduma.
- Idadi ya waliohudhiuria kliniki baada ya kujifungua ndani ya siku mbili na baadaye siku 3-7
- Idadi ya wanaotumia njia za kisasa uzazi wa mpango

Hakuna sababu ya kutofanya vizuri katika viashiria hivi na vingine ambavyo sijavitaja wakati tuna wadau wanatuwezesha kwa kila Halmashauri.

Ndugu washiriki,

Naomba kikao hiki kiwe cha kazi, pokeeni taarifa kutoka kila Halmashauri, zisikilize na kuzielewa vyema kisha jadili kwa kina na mwisho mtoke na maazimio ya kuboresha kwa kila eneo litakaloonekana lina changamoto.

Ninajua Afya ya Uzazi na mtoto inalenga kuzuia vifo vya mama na watoto na ninyi mnajua suala la vifo vinavyotokana

na matatizo ya uzazi kwa mama na mtoto halivumiliki na hivyo havikubaliki kwani Serikali inaimarisha miundo mbinu ya kutolea huduma za afya na pia upatikanaji wa watumishi na dawa. Niwaombe kila mmoja awajibike, watumishi pamoja na wadau tukishikamana mkoa wa Mara tutapiga hatua kubwa kusonga mbele.

Baaada ya kusema hayo, naomba nichukue fursa hii kusema kikao hiki kimefunguliwa rasmi.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.